

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



**OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA KIBITI**



Unapojibu tafadhali

Kumb.Na.KDC/KINY/016/13

Tarehe :03/04,2024

**TANGAZO LA NAFASI YA MWENYEKITI NA WAJUMBE WA BODI YA MFUKO
WA ELIMU WA WILAYA YA KIBITI (MARUDIO)**

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kibiti anawatangazia wananchi na wakazi wa Wilaya ya Kibiti nafasi 1 ya Mwenyekiti na nafasi 2 za wajumbe wa Bodi ya Mfuko wa Elimu wa Halmashauri ya Wilaya ya Kibiti.

2.0 NAFASI 1 YA MWENYEKITI WA BODI

2.1 Sifa za Mwombaji

- i) Awe raia wa Tanzania
- ii) Awe na umri usiopungua miaka 25 na asizidi 70
- iii) Awe na akili timamu
- iv) Awe na elimu ya Chuo Kikuu (angalau shahada ya kwanza)
- v) Asiwe na madaraka yoyote kwenye chama cha siasa
- vi) Asiwe mtumishi wa Halmashauri

3.0 NAFASI MBILI (2) ZA WAJUMBE WA BODI

3.1 Sifa za Mwombaji

- i) Awe raia wa Tanzania
- ii) Awe na umri usiopungua miaka 25 na asizidi 70
- iii) Awe na akili timamu
- iv) Awe na elimu ya Sekondari, yaani angalau kidato cha nne na kuendelea
- v) Asiwe na madaraka yoyote kwenye chama cha siasa
- vi) Asiwe mtumishi wa Halmashauri

4.0 Kazi za majukumu ya Bodi ya Mfuko wa Elimu zitakuwa kama ifuatavyo;

- a) Kubuni Mipango na Mikakati kwa ajili ya maendeleo ya elimu katika Halmashauri
- b) Kusimamia mgawanyo wa fedha kwenye shule kufuatana na bajeti iliyoidhinishwa na Mkutano Mkuu wa mwaka wa Bodi na kuridhiwa na Baraza la Halmashauri
- c) Kusimamia utekelezaji na kutathimini Mipango ya Elimu katika Halmashauri
- d) Kupitia na kurekebisha Mipango na Bajeti ya Elimu na kuwasilisha kwenye Mkutano Mkuu wa Mwaka wa utendaji kwa ajili ya kuidhinishwa
- e) Kupokea, kuchambua na kuidhinisha taarifa za utekelezaji wa Mfuko wa Elimu wa Halmashauri
- f) Kubuni vyanzo mbalimbali vya mapato na rasilimali za kutosha kuendesha Mfuko wa Elimu wa Halmashauri
- g) Kushirikiana na Kamati za Huduma za Jamii ya Halmashauri
- h) Kuratibu na kusimamia shughuli za maendeleo ya Elimu katika Halmashauri kulingana na program za kitaifa
- i) Kupitisha Kanuni za Utengaji na Utumiaji wa Fedha kutoka kwenye Mfuko kwa ajili ya kuendeleza madhumuni ya Mfuko
- j) Kusimamia ujenzi wa shule za Msingi, Sekondari na Vyuo vya Kati katika Halmashauri
- k) Kufanya jambo lolote litakalofanikisha maendeleo ya Elimu katika Halmashauri

Maombi yanaweza kuandikwa kwa lugha ya Kiswahili au Kiingereza na yatumwe kwa anuani ya Mkurugenzi Mtendaji (W), S.L.P 33 KIBITI kwa njia ya Posta au kwa kuleta mwenyewe ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Kibiti kabla au ifikapo tarehe 10/04/2024 saa 9.30 Mchana.

NB: Nafasi hizi hazina mshahara wala posho ya mwezi ila kutakuwa na posho ya vikao vya Bodi tu.


Hemed S. Magaro
Mkurugenzi Mtendaji (W)
KIBITI

MKURUGENZI MTENDA.JI
HALMASHAURI YA WILAYA
YA KIBITI
S.L.P 33
KIBITI-PWANI